



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MALIASILI NA UTALII
TAASISI YA UTAFITI WA MISITU TANZANIA



APRILI 14, 2021

TANGAZO LA KUITISHA MAANDIKO YA JARIDA LA TAFORI

Jarida la TAFORI linachapishwa Juni na Desemba kila mwaka. Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI) inatoa wito kwa Watanzania watakaopenda kuchangia kwa kuleta maandiko yenye taarifa za misitu na ufugaji nyuki kwa maendeleo ya Taifa kwa ajili ya Toleo la 11, Namba 2 litakalotoka Juni mwaka 2021. Mwandishi anaweza kuleta andiko lililoandikwa kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza.

Mada kuu za maandiko ya jarida hili ziwe katika maeneo yafuatayo:

- Usimamizi wa Misitu ya Asili na Ufugaji Nyuki;
- Misitu ya Jamii na Kilimo Misitu;
- Mashamba ya Miti na Uboreshaji Miti;
- Ukadiriaji/Tathmini wa Mazao ya Misitu na Nyuki;
- Kazi Misitu na Matumizi ya Misitu;
- Uhifadhi wa Nyuki wa Asali na Makazi yao
- Uhifadhi wa Nyuki Wasiong'ata na Makazi yao
- Uvunaji, Uchakataji na Ufungashaji wa Mazao ya Nyuki
- Viwanda na Huduma zinazohusiana na Ufugaji Nyuki
- Masoko ya Mazao ya Nyuki na Mfumo wa Masoko
- Uchumi-Jamii, Sera na Ugani; na
- Usimamizi na Usambazaji wa Taarifa za Misitu na Ufugaji Nyuki.

Muundo wa Maandiko ufuatae vigezo vifuatavyo:

A) Andiko

- Kichwa cha habari:** Kichwa cha habari cha andiko kinatakiwa kiwe kifupi na chenye kueleweka na kisichozidi maneno 20;
- Majina ya waandishi/ waandishi:** Majina ya mwandishi/ waandishi yanatakiwa kuandikwa kwa usahihi chini ya kichwa cha habari na yawe yenye wino mpana;
- Utangulizi:** Katika uandishi wa andiko lako unatakiwa uoneshe utangulizi wa andiko, ambapo pia unaweza ukaelezea historia fupi kuhusu andiko lako;

- iv) **Ujumbe muhimu na Dhima nzima:** Baada ya kumaliza kuandika utangulizi wa andiko lako, hakikisha kitakochofuatia ni ujumbe mkuu na dhima nzima ya uandishi wa andiko hilo;
- v) **Hitimisho na muendelezo:** Sehemu hii hufuatia baada ya dhima ya andiko lako na utahitajika kuweka hitimisho na suluhisho juu ya kilichoelezewa kwenye andiko lako.

B) Mitindo ya Uandishi

- i) **Fungamano na Fonti:**
Maandishi yote yanatakiwa yawe yemefungamana kushoto. Tumia fonti ya "Time New Roman" na ukubwa wa maneno uwe 12. Kumbuka kuwa ukubwa wa maneno wenye kipimo cha 10 utatumika kwenye majedwali tu;
- ii) **Aya:**
Ruka mstari mmoja kwa kila aya mpya;
- iii) **Mpangilio wa maneno na namba za kurasa:**
Tumia A4 kama kipimo cha kurasa, kingo zote nne za kurasa ziwe na urefu wa senti mita 2.5 na upana wa senti mita 2.5. Nafasi kati ya mstari mmoja hadi mwingine iwe 1.5. Jumla ya maneno katika andiko lako yasipungue 750 na yasizidi 1000;
- iv) **Majedwali:**
Katika uandaaji wa majedwari yako, weka akilini vipimo vya kurasa zako. Majedwali yote yanatakiwa kupewa namba na yawe na maneno elekezi katika mpangilio unaoeleweka. Vichwa vya habari vya majedwali vinatakiwa kuwekwa juu ya majedwali husika, mbele ya namba za majedwali hayo. Ni muhimu kuweka kumbukumbu ya wapi umetohoa majedwali uliyotumia endapo itakuwa umetumia jedwali kutoka kwenye andiko la mtu mwingine, na hii itaandikwa chini ya jedwali husika. Herufi ya kwanza ya kichwa cha habari cha jedwali ni lazima kiwe kwa herufi kubwa;
- v) **Vielelezo (Mf: takwimu, maumbo, michoro):**
Vielelezo vyote vinatakiwa viwe na namba, pia kuwe na maelezo yanayozungumzia hivyo vielelezo kwenye andiko lako. Vichwa vya habari vya vielelezo viwekwe chini ya vielelezo hivyo, baada ya namba ya vielelezo. Pia kichwa cha habari kinatakiwa kuanza na herufi kubwa. Idadi ya vielelezo (takwimu, maumbo, michoro) isizidi vinne (4). Picha zinaruhusiwa lakini hakikicha picha hizo zinaumiliki wako na sio picha za mmiliki mwingine kutoka kwenye mitandao; na
- vi) **Viambatisho:**
Viambatisho haviruhusiwi;

Uwasilishaji

Siku ya mwisho ya kuwasilisha maandiko ni Mei 14, 2021. Nakala laini za maandiko ziwasilishwe kwa Mhariri Mkuu – Jarida la TAFORI, S. L. P 1854, Morogoro, Tanzania. Barua pepe: tafori@tafori.or.tz. Hakikisha nakala inatumwa pia kwa Dkt. Siima Bakengesa, barua pepe: siima_b@yahoo.com; na Bw. Geoffrey Njovangwa, barua pepe: stargeof@gmail.com.

Imetolewa na,

Mhariri Mkuu